
Jarida la
HALMASHAURI YA
JIJI LA DODOMA

TOLEO NA. 019

# HERI YA MIAKA 59 YA MUUNGANO WA TANZANIA







**59** MIAKA YA MUUNGANO WA TANZANIA

1964 - 2023





# HISTORIA YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR

Na Theresia Nkwanga

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliundwa mnamo tarehe 26 Aprili, 1964 kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (inayojumuisha Visiwa vya Pemba na Unguja). Tanganyika ilikuwa ni mwendelezo wa koloni la Ujerumani, utawala wa Waingereza kwa Mamlaka ya Umoja wa Mataifa, Himaya ya Umoja wa Mataifa chini ya utawala wa Uingereza na mwisho Taifa huru kuanzia mwaka 1961 ndani ya nchi za Jumuiya ya Madola. Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ziliingia mkataba wa Muungano mnamo mwaka 1964 na kuanzishwa Dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkataba wa Muungano ulitiwa saini na aliyekuwa Rais wa Tanganyika, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Aprili 22, 1964 huko Zanzibar.

Mkataba huo ulithibitishwa na Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi hapo tarehe 26 Aprili, 1964. Tarehe 27 Aprili, 1964, viongozi wa nchi zote mbili walikutana katika ukumbi wa Karimjee Jijini Dar es Salaam na kubadilishana Hati za Muungano.




Sheria za Muungano zilitoa tamko la Jamhuri ya Muungano katika Ibara ya 4 kwamba: "Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar zitalazimika, baada ya kuungana na siku zote baada ya kuungana, kuunganishwa kuwa Dola ya Jamhuri kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar' (Ibara ya 4 Sheria za Muungano) Jina hili la "Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar" lilibadilishwa baadae mnamo tarehe 28 Oktoba, 1964 na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Sheria ya Jamhuri ya Muungano, Sheria namba 61 ya mwaka 1964.

## Muundo wa Muungano

Muundo wa Muungano wa Tanzania kama ulivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, una vyombo viwili vyenye mamlaka 3 ya utendaji ambavyo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki ambavyo ni Mahakama ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama ya Zanzibar na vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma ambavyo ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inashughulikia mambo yote ya Muungano kama yalivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanzania Bara. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inashughulikia mambo yote yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

## Sababu za kuwepo kwa Muungano

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umekuwepo kutokana na sababu mbalimbali kama vile:

Kuwepo kwa mahusiano ya karibu na ya kihistoria baina ya Tanganyika na Zanzibar katika nyanja mbalimbali kama vile udugu wa damu, biashara, utamaduni, lugha na mahusiano ya karibu kisiasa hususan baina ya vyama vya TANU na ASP.

Adhma ya kuwa na Muungano wa Afrika hususan kwa kuanzia na Shirikisho la Afrika Mashariki. Hata kabla ya uhuru wa Tanganyika, Mwalimu Nyerere pamoja na viongozi wengine waliokuwa wakipigania uhuru katika ukanda wa Afrika walikuwa na matarajio ya kuwa na Muungano wa Afrika. Mwalimu Nyerere binafsi alipendelea uwepo Muungano wa Afrika kwa kuanzia na Mashirikisho ya kikanda.

Kimsingi zipo sababu mbalimbali zilizosababisha Muungano huu kama vile historia za nchi hizi mbili, ukaribu wa nchi hizi mbili, muingiliano wa kijamii, ushirikiano wa kibiashara, ushirikiano madhubuti na wa muda mrefu wa kisiasa baina ya TANU na ASP, ushirikiano na urafiki wa muda mrefu kati ya watu, viongozi, na wakati wa harakati za utaifa uliopelekea uhuru wa nchi hizo mbili.

## Hati ya Makubaliano ya Muungano

Msingi wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ni Hati za Muungano za mwaka 1964. Hati za Muungano zilitiwa saini na waasisi wa Muungano tarehe 22 Aprili, 1964 na kupelekea Tanganyika na Zanzibar kuwa dola moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Baada ya Muungano, Mwalimu J. K. Nyerere alikuwa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya ya Muungano wa Tanzania na Sheikh Abeid Amani Karume, alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aprili 26, 1964 Bunge la Tanganyika lilipitisha Sheria za Muungano. Halikadhalika, Sheria hizi zilithibitishwa na Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

Sheria hizi za Muungano zilithibitisha Hati za Muungano, zilitaja Rais na Makamu wa Rais, zilitaja Muundo wa Muungano na Katiba ya Muungano. Aidha, Aprili 27, 1964 waasisi wa Muungano walibadilishana Hati za Muungano na wajumbe saba wa Baraza la Mapinduzi waliapishwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ni Sheikh Abeid Amani Karume, Kassim Abdala Hanga, Abdulrahaman Mohamed Babu, Hassan Nassor Moyo, Sheikh Aboud Jumbe, Hasnu Makame na Sheikh Idris Abdul Wakil. Baada ya kuapishwa kuwa Wabunge wakateuliwa kuwa Mawaziri wa Serikali ya Muungano.

Kabla ya Muungano, kulikuwa na Katiba ya Tanganyika ya mwaka 1962 na upande wa Zanzibar kulikuwa

na Amri za Katiba (Decrees).Katiba ya Tanganyika baada ya kufanyiwa marekebisho ili kukidhi mahitaji ya Muungano iliendelea kutumika kama Katiba ya Muungano ya mpito hadi mwaka 1977 ilipopitishwa Katiba ya Muungano kwa mujibu wa Makubaliano ya Muungano na Sheria za Muungano.
Aidha, marekebisho hayo yalimtaja Rais wa Zanzibar kuwa ni Makamu wa Kwanza wa Rais, akiwa ni msaidizi wa Rais kwa masuala yote ya kiutawala kwa upande wa Zanzibar, na Waziri Mkuu kuwa ni Makamu 5 wa Pili wa Rais ambaye atamsaidia Rais kwa masuala yahusuyo upande wa Tanganyika na kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.
Katiba ya muda ya mwaka 1965 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliainisha mambo kumi na moja ambayo yalikubalika kuwa ni ya Muungano chini ya usimamizi wa Serikali ya Muungano ambayo ni pamoja na Katiba na Serikali ya Muungano Mambo hayo ni: - Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi; Polisi ,Mamlaka juu ya mambo yanohusika na hali ya hatari, Uraia, Uhamiaji, Mikopo na Biashara ya Nchi za Nje na Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mambo mengine ni Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha, na Bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, posta na simu.

## Kuongezeka kwa mambo ya Muungano

Mambo ya Muungano yaliongezeka kutoka kumi na moja (11) hadi ishirini na mbili (22) kutokana na mahitaji ya ndani ya wananchi yaliyolenga kuunganika kwa mambo mengi zaidi pamoja na mabadiliko yaliyokuwa yanaendelea kutokea ulimwenguni baada ya Muungano.
Mwaka 1965 jambo la kumi na mbili linalohusu Mambo yote yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali (pamoja na noti), mabenki (pamoja na mabenki ya kuweka akiba) na shughuli zote za mabenki, fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusika na fedha za kigeni liliongezeka chini ya Katiba ya muda ya mwaka 1965.

Sababu kubwa ilikuwa ni kuwa na sarafu ya pamoja ya Tanzania baada ya Muungano, na kurahisisha usimamizi wa fedha za kigeni na mabenki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
Aidha, kufuatia kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, mambo matatu ya Muungano yaliongezwa, ambayo ni Leseni za viwanda na takwimu elimu ya juu, na usafiri na usafirishaji wa anga. Mwaka 1968, mambo ya maliasili ya mafuta, pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa na ama ya petrol na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa na gesi asilia yaliongezwa kwenye orodha ya mambo ya Muungano. 13 Aidha mambo ya Muungano yaliendelea kuongezeka hadi kufikia 21 kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977.
Mambo yote yaliyokuwa ya upande wa Tanganyika na Zanzibar yaliyokuwa yakisimamiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, yalikabidhiwa kwa Serikali ya Muungano. Mwaka 1992 kufuatia mabadiliko ya mfumo wa siasa nchini suala la ishirini na mbili la uandikishaji wa vyama vya siasa na mambo mengine yanayohusiana navyo liliongezwa kwenye orodha ya mambo ya Muungano.

## HITIMISHO

Muungano umechukuwa nafasi kubwa katika kuwaunganisha wananchi na kuimarisha mahusiano mazuri baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania imewek a wigo mpana kwa wananchi wake kuweza kuzitumia fursa mbalimbali zilizopo za kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa lengo la kujipatia maendeleo. Ni vyema tukatumia ipasavyo fursa zilizopo Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa kuleta maendeleo yatakayoinua hali ya uchumi wa Watanzania. Ili tuweze kuzitumia vizuri fursa hizi hatuna budi tuulinde, tuuimarishe na kuudumisha Muungano wetu adhimu kwani ni dira ya maendeleo na mafanikio yetu.







**Chanzo:** *Makala hii imeandaliwa kutoka katika vyanzo mbalimbali*





# Dkt. Samia aimwagia Dodoma Jiji Bilioni 14 za miradi





Na. Dennis Gondwe, DODOMA

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa shilingi 14,482,250,000 kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kuanzia sekta za afya, elimu, ardhi, viwanda hadi uwekezaji miradi iliyosaidia kuboresha huduma za kijamii.



Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru alipokuwa akiongelea mafanikio ya miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ofisini kwake.

Mafuru alisema katika kipindi cha serikali ya awamu ya sita, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa jumla ya shilingi 14,482,250,000 kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za Afya, Elimu, Ardhi na Viwanda, Biashara na Uwekezaji.



Aidha, Mheshimiwa Rais anaendelea kutekeleza miradi mingine mikubwa katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma ambayo ni ujenzi wa Barabara ya mzunguko, ujenzi wa reli ya kisasa ya mwendokasi na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato. Miradi yote hii imelenga kuboresha maisha ya wananchi.

Akiongelea sekta ya elimu, Mkurugenzi Mafuru alisema kuwa halmashauri yake ilipokea shilingi 3,520,000,000 kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 172 na samani zake.

Shilingi 954,000,000 zimepokelewa kutoka kwa wahisani wa SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Mtemi Chiloloma, mabweni mawili na madarasa mawili katika Shule ya Sekondari Bihawana. Mabweni mawili, madarasa mawili na madawati 60 katika shule ya sekondari ya wasichana ya Bunge alisema Mafuru.

Alisema kuwa shilingi 750,000,000 zimepokelewa kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwaajili ya ujenzi wa shule mpya ya mchepuo wa kingereza (Msangalale English Medium). Eneo lingine lililopokea fedha shilingi 858,250,000 ni kwa ajili ya uboreshaji miundombinu ya elimu ya msingi, aliongeza.

Mafuru alisema kuwa fedha zilizotolewa na serikali ya awamu ya sita kwa halmashauri yake ni nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Alisema kuwa fedha hizo zitaleta mapinduzi makubwa katika huduma za jamii na maendeleo ya watu na halmashauri yake. Aliahidi kuendelea kusimamia fedha hizo ili zilete matokeo makubwa na kuonesha thamani ya fedha kwenye miradi hiyo.

**Miaka 59 ya Muungano wa Tanzania**

**JIJI LA DODOMA**

# UJENZI WA KITUO CHA AFYA CHANG'OMBE

*MRADI UFADHILI WA SERIKALI KUU*







**MUONEKANO WA JENGO LA KITUO CHA AFYA CHANG'OMBE**

Ujenzi wa kituo cha Afya Chang'ombe unatekelezwa kwa fedha za tozo kutoka Serikali Kuu.

Fedha zilizotolewa mpaka sasa ni shilingi 500,000,000.00. Fedha zilizotumika ni shilingi 250,000,000.00 na zilizobaki ni 250,000,000.00.

Ujenzi wa Jengo la OPD, Maabara na Kichomea taka vimekamilika.

Ujenzi wa jengo la mama na mtoto, jengo la upasuaji (Theater) Uko hatua ya msingi

# Wana-Dodoma walipwa Bilioni 4 za fidia



Na. Dennis Gondwe, DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inajivunia kulipa fidia shilingi 4,174,722,894 kwa wananchi wa maeneo mbalimbali ambayo ardhi yao ilitwaliwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maedeleo katika kipindi cha miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru alipokuwa akiongelea mafanikio ya miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Jiji la Dodoma ofisini kwake.

Mkurugenzi Mafuru alisema katika kipindi cha miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita, chini ya uongozi wa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imelipa fidia jumla ya shilingi 4,174,722,894.25 kwa wananchi katika maeneo mbalimbali. Wananchi waliolipwa fidia ni katika maeneo ya Chigongwe, Nzuguni, Mbalawala na Dodoma Makulu pamoja na upanuzi wa eneo la Hoteli ya Jiji la Dodoma (Dodoma City Hotel).

Akiongelea umuhimu wa fidia hizo, alisema kuwa zinakwenda kubadilisha hali ya maisha ya wananchi na kuifanya kuwa bora zaidi. Fidia waliyopata wananchi baadhi yao wameweza kujenga nyumba bora, wengine wameweza kuboresha makazi yao na kufanya shughuli nyingine za maendeleo alisema.



Joseph Mafuru, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma

# Upatikanaji dawa, vifaa tiba waimarika

HALI ya upatikanaji dawa na vifaa tiba imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Katika kipindi cha awamu ya sita hali ya upatikanaji wa dawa katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeongezeka kutoka asilimia 84.6 hadi 91 kwa dawa muhimu.

Mganga Mkuu wa Jiji la Dodoma, Dkt. Andrew Method anasema ongezeko hilo la upatikanaji wa dawa muhimu unatokana na ongezeko la fedha za ruzuku za ununuzi wa dawa na vifaa tiba kutoka Serikali kuu.

Sambamba na ongezeko la ukusanyaji wa mapato kutoka katika vituo vya kutolea huduma kutoka asilimia 80 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 116 mwaka 2022. Makusanyo hayo yamepelekea kuimarisha upatikanaji wa vifaa tiba anasema Dkt. Method.





# Agizo la Rais kuhusu Machinga latimia Dodoma









Na. Dennis Gondwe, DODOMA

SOKO la wazi la Machinga kuliingizia Jiji la Dodoma mapato ya shilingi 1,780,368,000 kwa mwaka yatakayosaidia kuboresha huduma za jamii.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru alipokuwa akiongelea mafanikio ya serikali ya awamu ya sita kwa kipindi cha miaka miwili Jijini Dodoma.

Mafuru alisema kuwa ujenzi wa Soko la wazi la Machinga katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma umegharimu kiasi cha shilingi 9,529,747,200.66. Fedha zilizotumika katika ujenzi wa Soko la wazi la Machinga, shilingi 6,529,747,200 ni mapato ya ndani ya halmashauri, shilingi 2,500,000,000 ni ruzuku kutoka serikali kuu na shilingi 500,000,000 ni fedha kutoka mapambano dhidi ya Uviko -19.
Halmashauri ya Jiji la Dodoma tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha fedha katika kutekeleza mradi wa ujenzi wa Sko la wazi la Machinga alisema Mkurugenzi Mafuru.

Akiongelea mchango wa soko hilo la wazi, alisema kuwa soko hilo limewawezesha wafanyabiashara wadogo kufanya biashara zao katika mazingira bora na yenye staha.
Alisema kuwa halmashauri inatarajia kukusanya shilingi 1,780,368,000 kwa mwaka kutokana na maeneo ya kibiashara katika soko hilo.

# Miradi ya Mapato ya ndani yaanza kutoa matunda



Na. Dennis Gondwe, DODOMA

MIRADI ya maendeleo inayotekelezwa kwa mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeanza kutoa matunda kwa jiji hilo na kuchangia katika utoaji huduma bora kwa wananchi.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu wa Halmasahuri ya Jiji la Dodoma, Francis Kaunda alipokuwa akiongelea mafanikio ya miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais, Dkt. Samia Sulihu Hassan.

Kaunda alisema kuwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetekeleza miradi mingi ya maendeleo kwa mapato ya ndani ya halmashauri.

Mradi wa ujenzi wa hoteli ya Jiji la Dodoma (Dodoma City Hotel) umegharimu shilingi 11,945,995,952.50 ambazo ni mapato ya ndani ya halmashauri. Jengo hilo lina ghorofa 11, ikijumuisha vyumba 95 vya kulala, kumbi tatu za mikutano, mgahawa na bwawa la kuogelea katika ghorofa ya mwisho. Mradi unaingizia Halmashauri kiasi cha shilingi 600,000,000 kwa mwaka alisema Kaunda.

Akiongelea mradi wa jengo la kitegauchumi cha Jiji la Dodoma (Government City Complex - Mtumba) alisema kuwa mradi huo umegharimu kiasi cha shilingi 18,875,665,009.83.

Jengo la Hoteli lina ghorofa sita pamoja na maeneo ya maduka na sehemu ya kutolea huduma za fedha. Mradi una kumbi za mikutano saba. Ukumbi mmoja mkubwa wenye uwezo wa kuchukua watu 1,000 na kumbi ndogo sita zenye uwezo wa kuchukua watu 80 hadi 100 kila moja.



Hadi sasa mradi umeingiza shilingi 432,628,048.

Akifafanua kuhusu mapato yatokanayo na miradi hiyo ya maendeleo, alisema kuwa fedha hizo zinakwenda kuboresha huduma za kijamii katika jiji hilo.

Mradi huo unategemea kuingizia Halmashauri kiasi cha shilingi 1,999,128,048.00 kwa mwaka.



# Maboresho makubwa sekta ya Afya Dodoma



Na. Dennis Gondwe na Theresia Nkwanga, DODOMA

AFYA bora ni nguzo muhimu sana Katika kuhakikisha wananchi wana ukamilifu wa mwili, akili na kuepuka maradhi. Katika kipindi cha miaka miwili kumekuwa na kuongeza kwa idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya.

Serikali ya awamu ya sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan imejipambanua katika kuboresha huduma za Afya katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma ikiongeza vituo vya kutoa huduma za Afya kufikia 116.

Maendeleo ya taifa ni mchakato unaoanzia katika maendeleo ya mtu mmoja mmoja, familia, jamii hadi ngazi ya taifa. Ili dhana ya maendeleo iwe halisia na yenye maana suala la wananchi kuwa na afya njema haliwezi kupingika. Katika kuamini kwenye dhana hiyo miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita imejielekeza katika kuboresha sekta ya afya ili wakazi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Makao Makuu ya nchi wawe na afya bora.

Mkuu wa Divisheni ya Afya, Utawi wa Jamii na Lishe katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dkt. Andrew Method anasema katika miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan vituo vya kutolea huduma za Afya vimeongezeka kutoka vituo 100 mwaka 2020 hadi kufikia vituo 116 mwaka 2023. Kati ya vituo hivyo, Hospitali zipo saba, kati ya hizo hospitali mbili ni za serikali, Mashirika ya dini hospitali mbili, Mashirika ya Umma hospitali mbili, na watu binafsi Hospitali moja. Vituo vya Afya ni 12, kati ya hivyo, vituo vitano ni vya serikali, kimoja ni cha shirika la dini, vituo vitatu ni vya mashirika ya umma na vituo vitatu ni vya watu binafsi.

Ongezeko hilo linatajwa pia katika Zahanati. Zahanati zipo 81 ambazo zimegawanyika kama ifuatavyo; zahanati za serikali 37, mashirika ya dini 11, mashirika ya umma tisa, zahanati za watu binafsi 24. Kuna jumla ya kliniki maalumu 14 zinazomilikiwa na watu binafsi. Kituo cha uchunguzi kimoja (Diagnostic center) na maternity home moja anasema Dkt. Method.

Ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya limeenda sambamba na ongezeko la watumishi wa sekta ya Afya katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, katika kipindi cha miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita watumishi wameongezeka kutoka watumishi 472 hadi kufikia watumishi 509.



Ongezeko hilo linatokana na Halmashauri kupata watumishi wapya 37 wa sekta ya Afya sawa na ongezeko la asilimia nne ya watumishi wanaohitajika. Watumishi hao wamepangwa katika vituo mbalimbli vya kutolea huduma ili kuboresha utoaji wa huduma za afya katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Ama kwa hakika hakuna kama Mama, Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kutoa kipaumbele kwenye huduma za afya kwa kuboresha huduma na kuhakikisha zinawafikia wananchi wote alisisitiza Daktari Andrew



Miaka 59 ya Muungano wa Tanzania

# JIJI LA DODOMA

# Kizota, Zuzu, Nkuhungu wapata vituo vya Afya





HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inajivunia ujenzi wa vituo vitatu vya Afya katika kipindi cha miaka miwili ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa lengo la kusogeza huduma za Afya karibu zaidi na wananchi wake.

Katika awamu ya sita ya Serikali, Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilitenga kiasi cha shilingi 1,011,254,351.13 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vitatu vya Afya, zahanati na nyumba za watumishi wa sekta ya Afya.

Kiasi cha shilingi 639,806,668.00 kilitumika kujenga vituo vya Afya vitatu. Vituo vilivyojengwa ni kituo cha Afya Zuzu, Kizota na Nkuhungu.

Kituo cha Afya Kizota na Nkuhungu viko katika hatua za umaliziaji.

Ujenzi wa Zahanati ya Kiwanja cha Ndege, Soweto, Sogeambele, Ngambala na Zepisa kiasi cha shilingi 206,817,663.13 zimetumika.

Uendelezaji wa nyumba za watumishi Ipala, Chololo na Nzasa, jumla ya shilingi 30,000,000.00 zimetolewa. Aidha, ukarabati wa vituo vya Afya na zahanati ambapo kiasi cha shilingi 72,930,000.00 zilitumika.

Ununuzi wa samani katika vituo vipya vilivyofunguliwa umekamilika, ambapo kituo cha Afya Chang'ombe na Zahanati ya Makutopora kiasi cha shilingi 61,700,000 zimetumika.







# 500 wapata mafunzo njia bora uzalishaji Zabibu



Na. Prisca Maduhu na Josephine Kayugwa, DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imefanikiwa kutoa mafunzo ya njia bora za uzalishaji zabibu kwa wakulima 500 wa zabibu na maafisa ugani 25 ili waweze kuongeza uzalishaji na tija katika kipindi cha miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Divisheni ya Kilimo mjini Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Yustina Munishi alipokuwa akiongelea mafanikio ya miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ofisini kwake.

Munishi alisema kuwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma imefanikiwa kutoa mafunzo ya njia bora za uzalishaji wa zabibu kwa wakulima 500 na maafisa ugani 25. “Kampeni za kilimo zimefanyika na kuwafikia wakulima katika kata na mitaaa. Idadi wa wakulima waliofikiwa wanakadiriwa kuwa 12,200 ikilinganishwa na mwaka jana ambapo wakulima waliofikiwa wanakadiriwa kuwa 8,300. Aidha, miche 44,506 bora ya zabibu ilizalishwa na kugawiwa kwa wakulima bure” alisema Munishi.

Mafanikio mengine aliyataja kuwa ni kuwawezesha wakulima kupata mbegu za ruzuku za alizeti. “Kiasi cha tani 35 ziliuzwa kwa msimu wa mwaka 2021/2022 na kiasi cha tani tano zimeuzwa kwa wakulima msimu wa mwaka 2022/2023. Ruzuku hii ya mbegu za alizeti imesaidia kupungua kwa bei ya mafuta ya alizeti kutoka shilingi 9,000 kwa lita hadi shilingi 4,500 kwa lita” alisema Munishi.

Miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita imepata mafanikio katika kuwezesha upatikanaji wa mbolea ya ruzuku. Halmashauri ilisajili wakulima 10,270 kwa ajili ya kupata mbolea ya ruzuku kwa wakala waliosajiliwa kwa bei ya shilingi 70,000 badala ya shilingi 140,000, alisema.





# Jiji latoa Bilioni 7 Mikopo ya 10%

Na. Dennis Gondwe na Rajab Jumanne, DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imefanikiwa kukopesha mikopo isiyo na riba ya mapato ya ndani ya halmashauri kiasi cha shilingi 7,842,002,700 kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akiongelea mafanikio katika utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ofisini kwake, Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii na Vijana Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Charity Sichona alisema kuwa halmashauri imefanikiwa kuongeza mitaji ya biashara kwa wananchi, kuongeza kipato ndani ya familia, ajira na nguvu kazi kwa taifa kwa kufanya juhudi za kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Katika kipindi cha miaka miwili, halmashauri imekopesha jumla ya shilingi 7,842,002,700.00 ikiwa ni michango ya asilimia 10 Shilingi 4,010,795,151.00 pamoja na fedha za marejesho shilingi 3,831,207,549.00. Jumla ya Vikundi 643 vimenufaika ikijumuisha Wanawake 361, Vijana 222 na watu Wenye Ulemavu 60. Aidha, kumekuwa na ongezeko la urejeshaji mikopo kwa kuwa elimu ya umuhimu wa kurejesha inazidi kutolewa kwa vikundi vilivyokopeshwa. Hivyo, fedha za marejesho zimeongezeka kukopeshwa kutoka shilingi 966,305,650.00 hadi kufikia shiringi 1,765,421,784.28 alisema Sichona.








## Wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 Jiji la Dodoma











# Milioni 422 zakopeshwa kwa Machinga

Na. Dennis Gondwe na Rajab Jumanne, DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma katika miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanikiwa kutoa mikopo kwa vikundi 81 vya wafanyabiashara wadogo machinga shilingi 422,000,000 kwa lengo la kuwajengea mtaji wa kiuchumi ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii na Vijana, Charity Sichona alipokuwa akiongelea mafanikio ya miaka miwili ya serikali ya awamu ya sita kwa divisheni yake ofisini kwake.

Sichona alisema kuwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma imekuwa ikitoa kipaumbele kwa makundi maalum kwa kuyawezesha kiuchumi ili yatoe mchango wao katika uchumi.

Halmashauri ya Jiji imefanikiwa kujenga Soko la wazi la Machinga kwa ajili ya kuwawezesha wafanyabiashara ndogondogo zaidi ya 3,000 kufanya biashara katika mazingira salama na yenye staha. Aidha, imefanikiwa kuwapanga Machinga katika soko hilo na kuwapatia mikopo vikundi 81 yenye thamani ya shilingi 422,000,000 alisema Sichona.

Mkuu huyo alisema kuwa katika kuendelea kuyaimarisha makundi maalum mikopo ilikopeshwa kwa waendesha bodaboda na bajaji. Halmashauri ya Jiji imetoa mikopo kwa umoja wa waendesha bodaboda na bajaji yenye thamani ya shilingi 300,000,000. Hadi sasa shilingi 229,010,000 zimekwisha rejeshwa alisema Sichona.

Akiongelea uchangiaji wa asilimia 10 kutoka katika mapato ya ndani alisema halmashauri imefanikiwa kuchangia makusanyo halisi ya mapato ya ndani na kutoa fursa za mikopo nafuu isiyokuwa na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Asilimia nne ni ya wanawake, asilimia nne ya vijana na asilimia mbili ya watu wenye ulemavu. Halmashauri imeweza kuchangia asilimia 10 ya mapato halisi yaliyokusanywa alisema Sichona.

Alisema kuwa mwaka wa fedha 2020/2021 asilimia 10 ya mapato halisi ilikuwa 1,635,194,349.52 na fedha iliyochangiwa kwenye mfuko ilikuwa 1,635,194,349.52. Mwaka wa fedha 2021/2022 asilimia 10 ya mapato halisi 1,663,528,215.72 wakati fedha iliyochangiwa kwenye mfuko ni 1,663,528,215.72. Mwaka 2022/2023 asilimia 10 ya mapato halisi ni 1,347,330,421.38 na fedha iliyochangiwa kwenye mfuko ni 1,347,330,421.38. Hivyo, jumla ya shilingi 4,646,052,987 zilichangiwa kwenye mfuko alisema Sechona.








# MRADI WA UJENZI WA MADARASA MAWILI SHULE YA SEKONDARI ITEGA

*MAPATO YA NDANI*



Fedha zilizopokelewa: Shilingi 40,000,000
Chanzo cha fedha: Mapato ya ndani.

Ujenzi ulitumia 'force account'
Matumizi ya fedha: Shilingi 8,000,000 zilitumika kumlipa fundi na shilingi 32,000,000 zilitumika kununua vifaa vya ujenzi.
Hatua ya utekelezaji: Mradi umekamilika





Miaka 59 ya Muungano wa Tanzania

# JIJI LA DODOMA

## MRADI WA UJENZI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARASA SHULE YA MSINGI MBWANGA (KATA MNADANI)

*MAPATO YA NDANI*



Fedha zilizopokelewa: Shilingi 40,000,000
Chanzo cha fedha: Mapato ya ndani
Fedha zilizotumika: Shilingi 36,600,000
Fedha zilizobaki: Shilingi 3,400,000 zipo katika akaunti.
Hatua ya utekelezaji: Mradi umefikia hatua ya umaliziaji na vifaa vilivyokosekana ni vioo.





# HERI YA MIAKA 59

## MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR



JARIDA HILI LIMETOLEWA NA
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

**S.L.P 1249 DODOMA, TANZANIA**
**Baruapepe: cd@dodomacc.go.tz**
**Tovuti: www.dodomacc.go.tz**